

TANGAZO MAALUMU LA KUTUMA MAOMBI YA RUZUKU YA MIRADI MIDOGO MIDOGO INAYOSHUGHULIKIA MASUALA MBALI MBALI YA UTETEZI WA HAKI ZA WANAWAKE NA WASICHANA VIJANA WANAOTHIRIKA KATIKA MIKUTADHA YA WAKIMBIZI

Shirika la Women Fund Tanzania (WFT) lilianzishwa mwaka 2008 likiwa na lengo la kuchangia katika kuwawezesha Wanawake na wasichana, na hasa wale walio pembezoni mwa jamii zao kujijengea uwezo na sauti zaidi kwa kufikiwa na maarifa, ruzuku na kwa kuimarisha mikakati yao ya ujenzi wa nguvu za pamoja katika ngazi mbali mbali, na haswa kwenye ngazi za jamii.

Maudhui ya Tangazo Maalumu la Ruzuku

Kama sehemu ya mipango kazi yake ya mwaka huu, Shirika la WFT linakusudia kutoa ufadhili wa miradi midogo midogo kwenye mashirika yanayofanya kazi katika ngazi ya jamii yaliyojikita katika kukuza na kutetea haki za wanawake na wasichana na hasa wale waliopo katika mazingira ya wakimbizi. WFT inaamini kuwa ufadhili huu utachangia katika juhudi mbalimbali zinazoendelea katika kuleta mabadiliko ya kuondoa mifumo kandamizi, ikiwemo hali ya ukatili wa jinsia kwa wasichana na haswa wale wanaothariwa na muktadha wa hali ya wakimbizi nchini.

WFT inakaribisha maombi ya ruzuku ya miradi midogo ya utetezi wa haki za wanawake na vijana wa kike wanaothiriwa na hali ya ukimbizi, miradi hiyo isiwe na bajeti/ gharama inayozidi TSH 5,000,000- 7,000,000/=. Ruzuku hii itaangalia zaidi miradi iliyo katika mazingira yafuatayo:

- **Miradi inayolenga katika kukuza uelewa wa haki za wanawake na haswa wasichana wanaothirika na athari mbali mbali katika mikutadha ya wakimbizi kupitia ushiriki mpana na mijadala kuhusu haki ya elimu ya mtoto wa kike**
- **Miradi inayolenga kukuza na kujenga uwezo wa wanawake na wasichana wanaoathirika na mikutadha ya wakimbizi katika kukuza uelewa wa haki zao za msingi (Elimu, Afya, Uchumi, n.k.)**
- **Miradi inayolenga kukuza na kujengea uwezo wa mitandao ya wanawake inayopigania haki za wanawake na wasichana wakiwemo wanaoathirika na mikutadha ya wakimbizi kwa lengo la kukuza nguvu na sauti za pamoja katika ngazi mbali mbali**
- **Miradi inayolenga kukuza uelewa wa masuala ya Kijinsia kwa ujumla na haki za wanawake, wasichana wakimbizi**



Empowering Local Women Heroes

659 Mikoroshini Street, Namanga, Msasani
P.O.Box 79235 Dar es Salaam, Tanzania

+255 753 912 130
+255 22 266 4753

www.wft.or.tz

info@wft.or.tz

www.facebook.com/wft.tz
or @wft.tz

[@WomenFund_TZ](https://twitter.com/WomenFund_TZ)

[@WomenFund_TZ](https://www.linkedin.com/company/womenfund-tz)

Vifuatavyo ni vigezo vitakavyotumika wakati wa uchaguzi wa wazo bora la mradi

1. Ubora wa andiko la awali kuhusu mradi linaloonyesha uhusiano wa karibu kati ya tatizo lililopo, mikakati iliyopangwa pamoja na matokeo yanayotarajiwa.
2. Uwezo wa Shirika au Kikundi katika kutekeleza mradi wanaoomba.
3. Wazo la mradi linalo akisi ushirikishwaji wa wadau wa sekta mbalimbali katika kupanga na kutekeleza mradi hasa kwa kushirikishwa waathirika wakubwa wa athari mbalimbali katika mazingira ya wakimbizi, zikiwemo rushwa ya ngono au walioathiriwa na umaskini wa kiuchumi kwa njia mbali mbali.
4. Kujenga ubia kati ya mashirika ya kutetea haki za wanawake yanayolenga kuimarisha mitandao inayofanya kazi ya Kukuza haki za wanawake katika ngazi mbali mbali.
5. Muendelezo, na uwezo wa kuonyesha jinsi ya kuhifadhi na kutumia mifano mizuri ya utekelezaji katika ngazi za juu zaidi.
6. Ubunifu wa andiko la awali la mradi.

Muombaji wa ruzuku atafuata hatua mbili zifuatazo;

1. Uwasilishaji wa wazo la mradi (lisilozidi kurasa 5) likielezea mapendekezo/mawazo ya mradi huo na kuwasilishwa kabda ya tarehe **15 Desemba 2017**.
2. Baada ya uchambuzi kufanywa na kamati ya uchambuzi miradi, watakaochaguliwa watakaribishwa kuleta **andiko kuu la mradi**.

Tafadhali, **tumia miongozo/fomu zetu za wazo la mradi** kama inavyopatikana kupitia tovuti yetu: **www.wft.or.tz**. Fomu (miongozo) pia unaweza kutumwa Kwako kwa email pale itakapombwa au inaweza kuchukuliwa ofisi za WFT wakati wa saa za kazi.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 15 Desemba 2017, kwa kupitia barua pepe:**grants@wft.or.tz**; au WFT, kwa kupitia: S.L.P 79235, Dar es salaam. Pia maombi yanawezwa kupelekwa ofisi ya WFT ilioko: Mtaa wa Mikoroshini (Msasani) Nyumba namba 659 Dar es Salaam.

*** WATAKAO JULISHWAKUHUSU WALIOFANIKIWA KUPATA RUZUKU NI WALE TU WALIOCHAGULIWA, HIVYO KAMA IFIKAPO TAREHE 31 JANUARI, 2018, HUJAJULISHWA BASI ANDIKO LAKO HALIKUCHAGULIWA.**



Empowering Local Women Heroes

659 Mikoroshini Street, Namanga, Msasani
P.O.Box 79235 Dar es Salaam, Tanzania
+255 753 912 130
+255 22 266 4753

www.wft.or.tz
info@wft.or.tz
www.facebook.com/wft.tz
or @wft.tz

[@WomenFund_TZ](https://twitter.com/WomenFund_TZ)
[@WomenFund_TZ](https://www.linkedin.com/company/WomenFund_TZ)